

**Chanjo ya Homa ya
Ini ya B (Hepatitis B)**

Chanjo ya homa ya Hepatitis B inapendekezwa kwa watoto wachanga wote na inatoa kinga ya kudumu kwa maisha yote.

Mtoto wako mchanga anapaswa kupokea chanjo ya homa ya Hepatitis B katika umri ufuatao:

- Kuzaliwa
- Miezi 1 – 2
- Miezi 6 – 18

Chanjo: Hatua bora kwako katika kujikinga.

Ukiwa na maswali, muulize mtoa huduma wako wa afya.

**KWA TAARIFA
ZAIDI KUHUSU CHANJO
NA MAGONJWA, TEMBELEA**

- hhs.iowa.gov/public-health/immunization
- www.immunize.org
- www.cdc.gov/vaccines
- www.aap.org

Chanjo ya Hepatitis B

Chanja kwa maisha bora!



Health and
Human Services
Public Health



Health and
Human Services
Public Health

HOMA YA INI YA HEPATITIS B NI NINI?

Homa ya ini ya Hepatitis B (HBV) ni ugonjwa mbaya unaoshambulia ini na unaweza kusababisha ini kushindwa kufanya kazi, saratani ya ini na kifo. Hata hivyo, HBV inaweza kuzuiwa kwa chanjo yenye ufanisi na iliyo salama.

JE, WATU WANAPATA HOMA YA INI YA HEPATITIS B KWA NJIA GANI?

HBV hupatikana katika damu na majimaji ya miili ya watu walio na mambukizi ya Homa ya ini ya Hepatitis B. HBV inaweza kuenezwa kutoka kwa mama hadi mtoto wakati wa kuzaliwa. HBV pia inaweza kuenezwa kwa kushiriki:

- miswaki
- nyembe
- sindano zinazotumika kuchora chale na kutoboa tundu kwenye mwili
- kwa kufanya ngono bila kinga

Kugusana na hata kiasi kidogo cha damu iliyo na maambukizi hayo kunaweza kuambukiza. HBV haienezwi kwa kumnyonyesha mtoto, kukohoa, kupiga chafya, kukumbatiana au kupiga busu.

JE, NITAJUAJE KAMA NINA HBV?

Wanawake wote wajawazito wanapaswa kupimwa baada ya miezi mitatu ya kwanza ya kila ujauzito kwa kupima damu ili kuchunguza ikiwa kuna HBV. Hii ni hatua muhimu ya kuzuia kuenea kwa HBV hadi kwa mtoto wako wakati wa kujifungua. Mwombe mtoa huduma wako wa afya akupatie matokeo ya vipimo vyako vya HBV.

HAKIKISHA MTOTO WAKO ANAPATA CHANJO ANAPOZALIWA.

“Dozi ya wakati wa kuzaliwa” ni dozi ya kwanza ya chanjo ya homa ya ini ya Hepatitis B wanayopatiwa watoto wachanga mara tu baada ya kuzaliwa. Hii inafanywa ili kuzuia kupata HBV katika watoto wachanga pale wanapozaliwa. Homa ya ini ya Hepatitis B inaweza kusababisha maambukizi sugu ya ini, hivyo kusababisha hatari ya kuharibika kwa ini maishani na saratani ya ini. Dozi tatu za chanjo ya homa ya ini ya Hepatitis B itamkinga mtoto wako dhidi ya HBV. Chanjo ya homa ya ini ya Hepatitis B inapendekezwa na ni salama kwa watoto wachanga.

JE, CHANJO NI SALAMA?

Chanjo nchini Marekani ni salama na zenye ufanisi. Madhara ya kawaida yanayotokana na chanjo ni madogo na zinajumuisha uchungu kwenye eneo lililodungwa sindano ya chanjo au joto la kiwango cha chini. Dalili hizi ndogo ni za kawaida na zinapaswa kutarajiwa wakati mwili unapojenga kinga. Mimenyuko mikali ya mzio ni nadra sana. Yeyote anayepokea chanjo anapaswa kufahamishwa kikamilifu kuhusu manufaa na hatari zake. Maswali au wasiwasi wowote unapaswa kujadiliwa na mtoa huduma wako wa afya.



Watoto waliozaliwa na akina mama wenye HBV wanahitaji uangalizi wa ziada ili kuzuia maambukizi.

Watoto hawa wanahitaji globulini ya kinga dhidi ya homa ya ini Hepatitis B (HBIG) na vipimo vya ziada wakati wa umri ufuatao:

KUZALIWA:

Dozi ya wakati wa kuzaliwa ya chanjo ya homa ya ini Hepatitis B na dozi ua HBIG ndani ya saa 12

MWEZI 1 – 2:

Dozi ya 2 ya chanjo ya HBV

MIEZI 6:

Dozi ya 3 ya chanjo ya HBV

MIEZI 9 – 12:

Watoa huduma wanafanya vipimo vya damu ili kuthibitisha uwepo wa kinga dhidi ya HBV.

